**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**610** **UALIMU**

**Muda: saa 3** **Mwaka: 2020**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu **A, B, C, D** na **E** zenye jumla ya maswali **kumi na nane (18).**
2. Jibu Maswali yote katika sehemu **A** na swali **moja (1)** katika kila sehemu **B, C, D na E.**
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na kila sehemu **B, C, D na E** ina alama **kumi na tano (15).**
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhiswa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Eleza kwa kifupi kazi ya msingi ya matawi ya saikolojia yafuatayo:
   (a) Saikolojia ya elimu ya Jamii
   (b) Saikolojia ya makuzi
   (c) Saikolojia ya viwanda
   (d) Saikolojia ya unasihi.
2. Kwa kutumia hoja nne, bainisha umuhimu wa mwalimu kusoma saikolojia ya makuzi ya mtoto
3. Orodhesha mbinu kuu nne za unasihi
4. Eleza kwa kifupi maana ya maneno yafuatayo ya kisaikolojia:
   (a) Motisha
   (b) Kichocheo
   (c) Uhawilishaji wa mafunzo
   (d) Kichokoo halisi.
5. Kwa kutumia hoja nne, andika kwa kifupi umuhimu wa walimu kufanya matayarisho ya ufundishaji kabla ya kuingia darasani.
6. Eleza kwa kifupi vipengele vinne vya kuzingatia wakati wa kuandaa mwongozo wa usahihishaji.
7. Orodhesha mambo manne ya msingi ya kuzingatia wakati wa kufanya tathmini ya somo lolote.
8. Taja mambo manne yanayoweza kukwamisha utekelezaji wa elimu jumuishi katika shule za msingi Tanzania.
9. Kwa kutumia hoja nne, fafanua maudhui yaliyomo katika mtaala wa kufundishia katika shule za wamisionari.
10. Bainisha faida nne za kuwepo kwa Elimu Jumuishi nchini Tanzania.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU B ( alama 15)

Jibu swali **moja tu** katika sehemu hii

11. Chambua mbinu sita anazoweza kutumia mwalimu katika kuwamotisha wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
12. Eleza kasoro sita zinazosababisha mtoto kuwekwa kwenye kundi la kuvia akili.

## SEHEMU C (alama 15)

Jibu swali **moja tu** katika sehemu hii

13. Kwa kutumia hoja sita, onesha umuhimu wa utoaji wa mazoezi, majaribio na mitihani katika kufanikisha malengo ya kufundisha na kujifunza.
14. Chambua malengo sita ya sera mpya ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014

## SEHEMU D (alama 15)

Jibu swali **moja tu** katika sehemu hii

15. Maswali ya kuchagua jibu sahihi yana faida na hasara kwa mwalimu na mwanafunzi. Eleza kwa kina hoja hii kwa kuzingatia faida tatu na hasara tatu za maswali ya kuchagua jibu sahihi.
16. Eleza mambo sita ya kuzingatia wakati wa kumpima mwanafunzi kupitia shughuli za kiutendaji.

## SEHEMU E ( alama 15)

Jibu swali **moja tu** katika sehemu hii

17. Kila aina ya uongozi ina faida na hasara zake. Jenga hoja juu ya kauli hii kwa kutoa faida sita za uongozi wa kidikteta.
18. Kwa kutumia mifano, eleza kwa ufasaha mambo sita yanayoweza kufanya mwanafunzi mtu mzima asiwe na motisha ya kujifunza.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org